# DARASA LA SABA

**DISCOVERY CENSOR**

**DISCOVERY NATIONAL EXAMINATIONS**
**KCPE COMPLIANCE 2021**

# KISWAHILI SEHEMU YA KWANZA: LUGHA

**Muda:Saa 1 dakika 40**

## SOMA KWA MAKINI MAAGIZO YAFUATAYO

1. Umepewa kijitabu hiki cha maswali na karatasi ya kujibia. Kijitabu hiki kina maswali 50.
2. Ikiwa utataka kuandikia chochote ambacho si jibu andika katika kijitabu hiki.
3. Ukisha chagua jibu lako lionyeshe katika **KARATASI YA MAJIBU** na wala siyo katika kijitabu hiki cha maswali.

## JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU

4. Tumia penseli ya kawaida.
5. Hakikisha ya kwamba yafuatayo yameandikwa katika karatasi ya majibu:
   **NAMBA YAKO YA MTIHANI**
   **JINA LAKO**
   **JINA LA SHULE YAKO**
6. Kwa kuchora kistari katika visanduku vyenye namba zinazokusudiwa onyesha namba yako kamili ya mtihani (yaani namba ya shule, na zile namba tatu za mtahiniwa) katika sehemu iliyotengwa mwanzo wa karatasi ya majibu.
7. Usitie alama zozote nje ya majibu na usiikunje.
8. Iweke safi karatasi yako ya majibu na usikunje.
9. Kwa kila swali 1-50 umepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi A, B, C na D.
   Ni jibu **MOJA** tu kati ya hayo manne ambalo ni sahihi. Chagua jibu hilo.
10. Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi lionyeshwe kwa kuchora kistari katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndilo jibu.

**Mfano**

19. Tumia kiambishi sahihi.
    Darasa __ tajengwa kesho.
    A. i B. u C. li D. ki

**Jibu sahihi ni C**
**Katika karatasi ya majibu**

9 [A] [B] [C] [D] 19 [A] [B] [C] [D] 29 [A] [B] [C] [D] 39 [A] [B] [C] [D] 49 [A] [B] [C] [D]

Katika visanduku vinavyoonyesha majibu ya swali namba 19, kisanduku chenye herufi C ndicho kilichochorwa kistari

11. Chora kistari chako vizuri. Kistari chako kiwe cheusi na kisijitokeze nje ya kisanduku.
12. Kwa kila swali, chora kistari katika kisanduku kimoja tu kati ya visanduku vinne ulivyopewa.

UGUNDUZI

*Discovery Educational Publishers. Nairobi*

**Kijitabu hiki cha maswali kina kurasa 8 zilizopigwa chapa.**

*Discovery National Examinations 2021*

GEUZA UKURASA

***Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 hadi 15. Kwa kila nafasi, umepewa majibu manne. Jaza kila pengo kwa jawabu lifaalo zaidi.***

____ jambo linaloridhisha kama kujua kuwa ___2___ katika hatari ya kuangamizwa na virusi __3___ ukimwi. ___4__ utawasikia watu ___5___ wenzao wanaohitaji kwenda kwenye vituo vya kupimwa kwa kuwaambia __6__ wakaambukizwa maradhi yale kule. Nao wenye kuambiwa huzidi __7__ maisha yao na mwishowe huishi bila kupimwa. Hali ___8___ huwafanya kujawa na mawazo __9__.

| | A | B | C | D |
|---|---|---|---|---|
| **1.** | A. Haipo | B. Haupo | C. Halipo | D. Hampo |
| **2.** | A. haupo | B. hupo | C. hukui | D. haukui |
| **3.** | A. za | B. ya | C. cha | D. vya |
| **4.** | A. Aghalabu | B. Hata | C. Kwa kuwa | D. Mara nyingi |
| **5.** | A. wakiwatamani | B. wakitamauka | C. wakitamani | D. wakiwatamausha |
| **6.** | A. huenda | B. ikawa | C. iwapo | D. mara nyingi |
| **7.** | A. huhofu | B. kuogofya | C. huhofia | D. kuogopea |
| **8.** | A. hizi | B. hiyo | C. hii | D. hilo |
| **9.** | A. shelabela | B. riboribo | C. mzozo | D. mpwitompwito |

Ukweli ni kwamba, baadhi nyumba zinazobomoka na kuwafunika watu kwa ___10___ ni zile ambazo ziliwekwa msingi __11___. Ni ___12___ wa kila ___13___ kuyajali maisha ya watu watakaoishi ___14___ majengo ___15___.

| | A | B | C | D |
|---|---|---|---|---|
| **10.** | A. virusi | B. vijusi | C. vijuzi | D. vifusi |
| **11.** | A. dhalili | B. dalili | C. nadhifu | D. fadhili |
| **12.** | A. jukumu | B. wajibu | C. wadhifa | D. wahaka |
| **13.** | A. mkazi | B. mwasi | C. mwashi | D. mwanzi |
| **14.** | A. katika | B. kwenyewe | C. katikati | D. kati ya |
| **15.** | A. haya | B. hizo | C. hiyo | D. hayo |

**_Kutoka swali la 16 hadi 30, jibu kulingana na maagizo._**

16. *Andika wingi wa;*
Chungu hiki kina chungu.
A. Vyungu hivi vina vyungu
B. Chungu hivi vina vichungu
C. Vyungu hivi vina chungu
D. Chungu hivi vina machungu

17. Kitenzi ***'tokota'*** katika hali ya kutendesha kitakuwa ni;
A. kukoswa
B. tokosa
C. tokoka
D. tokosatokosa

18. Damu ni kwa jeraha kama vile ___ ni kwa jipu.
A. usaha
B. nta
C. matongo
D. koga

19. *Jibu kitendawili hiki;*
Kitu kidogo kimemtoa mfalme kitini pake pa enzi.
A. Malkia
B. Haja ndogo
C. Maumivu
D. Rununu

20. Maneno yaliyo katika ngeli ya **U-U** ni;
A. wino, uji, werevu
B. uyoga, unywele, wema
C. uso, ubua, ugali
D. waya, wali, uongo

21. *Kamilisha kwa usahihi.*
_____ ndizi.
A. Chane ya
B. Fungu la
C. Mkungu ya
D. Kichala cha

22. Chagua vazi la kike linalovaliwa kuanzia mabegani na kuishia magotini.
A. Kanchiri
B. Kizibao
C. Shimizi
D. Gaguro

23. Kanusha sentensi ifuatayo;
Njoo hapa!
A. Usinjoo hapa!
B. Nenda pale!
C. Nenda kule!
D. Usije hapa!

24. Viluwiluwi wa mbu husababisha malaria ilhali mbung'o husababisha;
A. matende
B. tauni
C. malale
D. kichocho

25. Robo tatu katika tarakimu huandikwaje?
A. $^{3}/_{7}$
B. $^{3}/_{4}$
C. $^{3}/_{6}$
D. $^{3}/_{8}$

26. *<u>Kamilisha tashbihi.</u>*
Kinara alikuwa ametulia;
A. tuli
B. kama mwanakondoo
C. katika aliye usingizini
D. kama mfungwa

27. Ipi si nomino - **ambata**?
A. mastakimu
B. mjamzito
C. kifauongo
D. mwenyekiti

28. Chagua kisawe cha neno bahili.
A. muongo
B. mfitini
C. mjinga
D. kisangati

29. <u>Ndovu walivamia shamba letu.</u>
*Katika ukubwa na wingi ni;*
A. Madovu yalivamia majishamba yetu
B. Kidovu kimevamia mashamba yetu
C. Madovu yamevamia majishamba zetu
D. Ndovu zimevamia mashamba zetu

30. Wakati baina ya saa sita na saa nane ni adhuhuri watu hula;
A. kiamsha kinywa
B. kishuka
C. kijio
D. mwiku

***Soma ufahamu ufuatao kisha ujibu maswali 31 hadi 40.***

Kuna kazi mbalimbali ulimwenguni. Kuna ualimu, udaktari, urubani, unahodha nikitaja chache tu. Aidha, kuna kazi ya uganga. Utakubaliana nami katika pitapita zako umeona vibao vingi vikitangaza waganga maarufu, vingine vimegongomelewa mitini na kujiinamia tu. Je wanaoandika wamesahau kuwa chema chajiuza na kibaya chajitembeza?

Uganga si kazi ambayo mtu hurithi kwa siku moja. Mara nyingi utakuta mtu aliye mjuzi wa uganga ni yule ambaye ameinukia katika mazingira ya uganga. Hivyo ukipeleleza zaidi utakuta kwamba baba yake au babu yake au hata jamaa yake nzima inatokana na ukoo ambao umepata mazingira ya kiganga.

Elimu ya uganga basi ni ya miaka na mtu hawezi kujiita mganga baada ya siku chache za kuutalii. Linalosikitisha zaidi ni jinsi waganga wamezuka kwa fujo. Wao hujipa majina makubwa makubwa na kutaja uwezo wao wa kusuluhisha kesi, kuondoa utasa na ugumba na kutoa nafasi za madaraka kazini. Jambo hili ni hatari kwani huenda likawapotosha wengi wanaodhani ni ukweli. Wakifika pale huitishwa kifungua mkoba na ada pia.

Si kwamba waganga wote ni bandia; kuna wale halisi kwani hata enzi za babu zetu wao ndio waliotibu ndwele ainati kwa kutumia mitishamba. Hata hivyo tusipapie mambo bila ya kuyachunguza na kukimbilia yeyote anayekuja kwa kuwa twaweza kuyaweka maisha yetu hatarini.

**31.** Kulingana na habari hii kazi ya uganga;
A. hurithiwa na kizazi hadi kingine
B. ni kazi ngumu sana
C. ni somo la muda mfupi
D. si jambo la kurithiwa na watoto pacha

**32.** Kinyume cha kuganga ni;
A. kugangua
B. kudhuru
C. kuokoa
D. kurithi

**33.** Mwandishi anasema ili uwe mganga halisi;
A. upate mafunzo yauganga chuoni
B. ufanye usuhuba na waganga
C. ukulie katika mazingira ya kiganga
D. ujitangaze ili uweze kujulikana

**34.** Vibao vya kutangaza waganga vimegongelewa mitini kwa kutumia ___ inayotumiwa kugongomelea misumari.
A. kinoo
B. nyundo
C. tupa
D. mbao

**35.** <u>Waganga wamezuka kwa fujo.</u> Hii inamaanisha;
A. ni wengi
B. ni wachache
C. kiasi
D. maradufu

**36.** <u>Ukipeleleza zaidi</u>..... badala ya kutumia maneno haya waweza kutumia semi;
A. kupiga chenga
B. kupiga hatua
C. kupiga miayo
D. kupiga darubini

**37.** Waganga husema wanaweza kusuluhisha utasa na ugumba ili watu wapate;
A.wakembe
B. mamlaka
C. kazi
D. mali

**38.** Mwandishi anatutahadharisha dhidi ya;
A. kutibiwa na waganga wote
B. kuwa na papara bila kuchagua mambo
C. kulipa ada kwa waganga
D. kupata madaraka kazini

**39.** Malipo kwa mganga ni <u>ada</u> nayo zawadi kwa kumshika mtoto ni;
A. fola
B. mukafaa
C. maduhuli
D. fichuo

**40.** Kichwa mwafaka cha habari hii ni;
A. Waganga wote ni halisi
B. Waganga wa mitishamba
C. Waganga na waganguzi
D. Maprofesa bandia

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 41-50.***

Alijulikana kwa jina Zainabu Bati. Kila mja shuleni pao alimfahamu vizuri sana japo alikuwa mwanafunzi mnyamavu, mpole na asiyependa makeke na vishindo. Mambo yake yalikuwa taratibu na yaliyoratibiwa yakaratibika. Michezo mingi ya kubananga wakati na isiyo na maana hakuicheza. Ungempata katulia tuli darasani akibukua hasa wakati mgambo ilipokuwa imelia na wengi wakawa mbioni kufanya maandalizi kabambe.

Tangu hapo awali alipokuwa katika darasa la sita na saba, alikuwa miongoni mwa wale ambao walitunzwa kila mwisho wa muhula kwa kufanya vizuri katika mitihani ya darasa. Aliuthamini sana ushirikiano wa wanafunzi wenziwe darasani, hasa wale waliokuwa na chudi kama yeye. Mizozo ya kitoto darasani na wanafunzi waliopenda kulaza damu usingempata akijihusisha nayo kwani hakupenda kuumana meno na yeyote.

Alipofika darasa la nane aliendelea kushikilia uzi ule ule. Bila shaka aliamini kuwa atangaye sana na jua hujua. Naam! Hakukosea. Miezi kadhaa ya papo kwa hapo hatimaye jiwe lilikatika. Matokeo ya mtihani yalipotangazwa, la ibura lilitendeka. Kila mja hapo shuleni pao alijua kuwa banati Zainabu angepita mtihani.

Hata hivyo hakuna aliyefikiria kuwa angekuwa katika orodha ya wanafunzi mia moja bora katika taifa zima na jina lake kuchapishwa gazetini.

Alimiminiwa sifa tumbitumbi na kila mtu, si walimu, si wazazi, si wakurugenzi na hata wanafunzi wenzake. Alipoitwa kujiunga na shule ya wasichana ya Alliance, ilikuwa ni fahari kubwa kwa kila mtu aliyehusishwa naye. Shabash! Achanikaye kwenye mpini hafi njaa.

**41.** Ni ipi kati ya sifa zifuatazo sio sifa ya Banati , Zainabu kulingana na kifungu?
A. Bidii
B. Mnyamavu
C. Mpole
D. Mjuvi

**42.** Kubananga wakati ni kifanya nini?
A. Kumaliza wakati
B. Kutumia muda
C. Kucheza na masomo
D. Kuharibu muda

**43.** 'Ungempata ametulia tuli....' <u>Tulia tuli</u> ni;
A. tanakali ya sauti
B. kihusishi
C. tashbihi jozi
D. takriri

**44.** Zainabu aliuthamini sana ushirikiano na wenzake. Ni methali gani asiyoelezea hali hii?
A. Upweke ni uvundo
B. Mwenye pupa hadiriki kula tamu
C. Mkono mmoja hauchinji ng'ombe
D. Kinga na kinga ndipo moto uwakapo

**45.** 'Wanafunzi waliokuwa na chudi kama yeye... inamaanisha __
A. waliokuwa na zohali
B. waliokuwa na ajizi
C. waliokuwa na jitihada
D. waliosoma sana

**46.** Ni kauli gani sahihi kulingana na ufahamu?
A. Zainabu ndiye aliyetunzwa pekee kila mwisho wa muhula
B. Zainabu alipofika darasa la nane aliendelea kulaza damu
C. Zainabu aliwashangaza wengi kwa matokeo yake duni
D. Zainabu alijiunga na shule tajika

**47.** Tukio gani la ajabu lililotendeka?
A. Zainabu kupasi mtihani wake
B. Zainabu kukataa kujiingiza katika mizozo ya kitoto
C. Zainabu alipozidi matarajio ya wengi kwa kuupita mtihani wake vizuri zaidi
D. Jina lake Zainabu kuchapishwa gazetini

**48.** Kamilisha methali; Mchuma janga;
A. hula na wa kwao
B. hulia kivulini
C. hulilia uvulini
D. hula jangale

**49.** Jambo la ibura ni;
A. Jambola kuzingatiwa
B. Jambo lisilotarajiwa
C. Jambo la kushangaza
D. Jambo la kuhofisha

**50.** Kichwa mwafaka cha ufahamu huu kinaweza kuwa;
A. Mteuzi heshi tama
B. Riziki mikononi mwa waja
C. Jitihada haiondoi kudura
D. Mchumi haozi